

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MAJI**



**USAJILI WA TAASISI, KAMPUNI NA WATAALAM BINAFSI WANAOFANYA KAZI  
ZA UTAFITI NA UCHIMBAJI WA VISIMA VYA MAJI CHINI YA ARDHI KWA  
MUJIBU WA SHERIA YA USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA MAJI NA.11 YA  
MWAKA 2009 PAMOJA NA MAREKEBISHO YAKE NA. 8 YA MWAKA 2022**

Wizara ya Maji inazitaka Taasisi, Kampuni na Watu binafsi wanaofanya kazi za utafiti na Uchimbaji wa maji chini ya ardhi ambao bado hawajajisajili, kuhakikisha wanajisajili ndani ya siku thelathini (30) kuanzia tarehe ya tangazo hili.

Kufanya kazi za utafiti na uchimbaji wa visima vya maji chini ya ardhi bila ya kusajiliwa na Wizara ya Maji ni kosa linalopaswa kuadhibiwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2022.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa simu nambari: +255 713 396 591 au kwa barua pepe: [dwr@maji.go.tz](mailto:dwr@maji.go.tz), au fika katika ofisi za Idara ya Rasilimali za Maji zilizopo Barabara ya Ali Hassan Mwinyi karibu na Ofisi za Makao Makuu ya Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA). Pia, unaweza kufika kwenye Ofisi za Bodi za Maji za Mabonde na Ofisi ndogo za Bodi za Maji za Mabonde zilizopo katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

Dkt. George V. Lugomela

**MKURUGENZI  
IDARA YA RASILIMALI ZA MAJI**

Wizara ya Maji,  
Idara ya Rasilimali za Maji,  
Makao Makuu Dodoma,  
**41104 Tambukareli, DODOMA**



[www.maji.go.tz](http://www.maji.go.tz)



[dwr@maji.go.tz](mailto:dwr@maji.go.tz)